viii) Ni wajibu wa mshitakiwa kupokea wito na kuhudhuria katika Baraza hata kama anao uthibitisho wa uhalali wa umiliki wake katika ardhi ama nyumba yenye mgogoro;

ix) Mdaiwa anaposhindwa kuhudhuria barazani (bila taarifa yoyote ya maandishi ikiambatana na vielelezo) anakosa nafasi ya kusikilizwa na upo uwezekano wa kushindwa kesi kwani hukumu itatolewa kwa kuzingatia maelezo ya upande mmoja;

x) Anayefungua shauri ama Mshitakiwa (wadaawa) katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya anaweza kujiwakilisha mwenyewe ama kutafuta mwanasheria wa kumwakilisha katika shauri husika.

xi) Mdaiwa baada ya kupokea nakala ya madai/mgogoro wa ardhi anawajibika kuwasilisha ndani ya siku 21 majibu ya madai ya mgogoro uliowasilishwa dhidi yake katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya. Majibu kwa maombi madogo (Miscellaneous Application) ni lazima yawasilishwe barazani ndani ya siku 14;

xii) Shauri katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya halitaanza kusikilizwa kabla ya majibizano ya awali kwa njia ya maandishi (pleadings) kukamilika;

xiii) Ni wajibu kwa wadaawa kuambatisha vielelezo vyote muhimu vilivyopo kwenye majibizano yao ya awali ya maandishi (pleadings) kabla shauri halijaanza kusikilizwa;

xiv) Kabla shauri halijaanza kusikilizwa ni wajibu kwa wadaawa kuainisha / kutaja idadi ya mashahidi watakaofika kwenye Baraza kwa ajili ya kutoa Ushahidi;

xv) Kila upande katika shauri unayo haki ya kusikilizwa na kuwasilisha vielelezo pamoja na mashahidi wakati wa usikilizaji wa shauri;

xvi) Kila upande unayo haki ya kuuliza maswali kwa upande wenye zamu ya kutoa maelezo yake/Ushahidi;

xvii) Uamuzi/Hukumu ya Baraza haiwezi kutolewa kabla ya kumaliza kusikiliza pande zote isipokuwa pale ambapo mshitakiwa hajahudhuria itatolewa hukumu ya upande mmoja;

xviii) Upande ambao hautaridhika na uamuzi/hukumu ya Baraza unayo haki na nafasi ya kukata rufaa kwenda Mahakama Kuu ya Tanzania Kitengo cha Ardhi ndani ya siku 45 baada ya uamuzi/hukumu kusomwa;

xix) Upande ambao unakusudia kukata rufaa kwenda Mahakama Kuu unaweza kuwasilisha maombi madogo Barazani kuomba zuio la utekelezaji wa hukumu kabla muda wa kukata rufaa kuisha *(Application for Stay of Execution);*

xx) Gharama za kuendesha shauri katika Baraza la Ardhi zinabebwa na wadaawa wenyewe ikiwemo gharama za kumlipa dalali endapo atateuliwa kwa ajili ya utekelezaji wa uamuzi/hukumu ya Baraza;

xxi) Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya linaweza kutoa amri ili upande ulioshindwa kesi uweze kumlipa mshindi gharama za kuendesha shauri.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI**

# MAJUKUMU YA MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA

SCAN ME

*Mawasiliano ya Wizara*
*Address: S.L.P. 2908, Dodoma.*
*Barua Pepe: ps@lands.go.tz*
*Simu: +255 26 296 3313 / +255 26 296 3314*
*Nukushi: +255 26 296 3316*

## UTANGULIZI

Serikali kupitia Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995 na Sheria za Ardhi za mwaka 1999 (Sura ya 113 na 114) ilianzisha mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini. Sera na Sheria hizo zilifuatiwa na Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Sura ya 216. Mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi ulianzishwa ili kuwa na vyombo rafiki vinavyoshirikisha jamii katika utatuzi wa migogoro ya ardhi.
Katika kutekeleza matakwa ya Sheria za Ardhi za mwaka 1999,Wizara ilianzisha Kitengo cha MABARAZA ambacho kinatekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Sura ya 216 katika kusimamia utendaji kazi wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya. Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ni chombo maalum kilichoanzishwa na serikali kwa lengo la kushughulikia migogoro ya ardhi katika ngazi za wilaya kote nchini.

## LENGO KUU LA KITENGO CHA MABARAZA

Lengo Kuu la Kitengo cha MABARAZA ni kuratibu na kusimamia uadilifu, uwajibikaji, uwazi, haki na ubora katika kushughulikia utatuzi wa migogoro ya ardhi inayowasilishwa katika Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.
Katika kuhakikisha kwamba wananchi wanapata huduma ya utatuzi wa migogoro ya ardhi, Wizara imeanzisha Mabaraza 117 ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yanayotoa huduma kote nchini. Lengo la Wizara ni kuhakikisha kuwa Wilaya zote 139 zinakuwa na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya ili kuwasogezea wananchi huduma iliyo karibu.

## MAJUKUMU YA KIMAHAKAMA YANAYOTEKELEZWA NA MABARAZA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA

*(Kifungu cha 33 cha Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Sura ya 216)*

Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya yamepewa mamlaka kushughulikia migogoro ya ardhi inayohusiana na:

a) Umiliki wa Ardhi;
b) Mipaka baina ya majirani wamiliki wa ardhi;
c) Ardhi/Nyumba iliyowekwa rehani katika taasisi za fedha; na
d) Mikataba ya Upangaji/Upangishaji wa Nyumba/Ardhi.

## MAMBO MUHIMU YA KISHERIA YA KUZINGATIA UNAPOFUNGUA SHAURI LA ARDHI KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA

*(Kifungu cha 29-36 cha Sheria ya Mahakama za Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi Sura ya 216)*

i) Mgogoro wa ardhi unaoweza kuwasilishwa katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ni ule tu unaohusu ardhi ama nyumba yenye thamani isiyozidi shilingi milioni mia tatu (300,000,000);

ii)Mgogoro wa ardhi ama nyumba yenye thamani inayozidi shilingi milioni mia tatu (300,000,000/=) unapaswa kuwasilishwa Mahakama Kuu ya Tanzania Kitengo cha Ardhi;

iii) Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya halina mamlaka ya kupokea na kushughulikia Mgogoro wa ardhi ama nyumba unaohusu Serikali za Mitaa ama Serikali Kuu;

iv) Mgogoro wa ardhi ama nyumba unaohusu Serikali za Mitaa ama Serikali Kuu unapaswa kuwasilishwa Mahakama Kuu ya Tanzania Kitengo cha Ardhi;

v) Ni lazima kuwasilisha mgogoro husika kwa ajili ya usuluhishi na kupata cheti cha Usuluhishi katika Baraza la Kata kabla ya kufungua shauri katika Baraza la Ardhi na Nyumba;

vi) Ni lazima kuwasilisha maombi maalum kwa mujibu wa sheria *(Main Application/Miscellaneous Application)* yanayoelezea mgogoro husika;

vii) Anayefungua shauri katika Baraza ana wajibu kuhakikisha kuwa mshitakiwa anapokea wito na kisha kuwasilisha mrejesho barazani wa namna wito ulivyopokelewa ama kutopokelewa;